# Kitenzi Kisaidizi na Kitenzi Kishirikishi katika Lugha ya Kiswahili

■ Dr.Abdalla M. Aghel*

● Received: 15/01/2024 ● Accepted:07/03/2024

■ **Ikisiri:**

Makala hii imelenga kutambulisha vitenzi katika lugha ya Kiswahili na aina zake, uamilifu wa kila kitenzi, na mfanano na tofauti kati yake. na imebaini kwamba kuna aina tatu za vitenzi hivyo: vitenzi vikuu, vitenzi visaidizi na vitenzi vishirikishi na ilionyesha tofauti kati ya vitenzi visaidizi na vitenzi vishirikishi. na pia ilieleza kuwa Kitenzi kisaidizi Ni kipengele cha neno au maneno kinachosaidiana na kitenzi kikuu ili kitendo kilichotendwa kifafanuliwe au kieleweke zaidi yaani, Vitenzi visaidizi vinaunga mkono kitenzi kikuu katika sentensi. Kinachojulikana kama kitendo shirikishi ni kitendo kinachoonyesha umoja wa mambo katika hali, tabia, au katika mazingira sawa. Kazi za kitenzi kishirikishi ni Geuza kitenzi kuwa kivumishi ili kurekebisha nomino, pia Unganisha na vitenzi visaidizi ili kuunda nyakati tofauti, kama vile njeo timilifu iliyopo, Aidha Kuonyesha cheo au kazi anayofanya mtu na sifa zake pamoja na kuonyesha umoja wa vitu au watu na mahali.

● **Key words**: vitenzi, vitenzi visaidizi, vitenzi vishirikishi, kivumishi.

■ المستخلص:

تهدف هذه المقالة إلى التعريف بالأفعال في اللغة السواحيلية وأنوعها، ووظيفة كل فعل منها وأوجه التشابة والاختلاف فيما بينها ،كما أوضحت المقالة بأن هناك ثلاثة أنواع للأفعال هي الأفعال الرئيسية والأفعال المساعدة وأفعال الكينونة وأشارت إلى الاختلاف بين الأفعال المساعدة وأفعال الكينونة وأوضحت أيضا بأن الفعل المساعد فهو الفعل الذي يأتي لكي يساعد الفعل الأساسي. بمعنى أنه يكون

. * *lecturer at the Department of Afro-Asian Languages, College of languages – University of Tripoli.
Email:ab.aghel@uot.edu.ly

الفعل الثاني بالجملة ولا يأتي الفعل المساعد لوحده في الجملة، لأنه في هذه الحالة يكون فعلاً أساسياً وهو يساعد الفعل الرئيسي في حالتي النفي والإثبات.

أما مايعرف بالفعل الكينونة هو فعل يعبر عن وحدة الأشياء في حالة أو سلوك أو في نفس البيئة، تعمل أفعال الكينونة في اللغة السواحيلية على تحويل الفعل إلى صفة لتعديل الاسم، وكذلك دمجه مع الأفعال المساعدة لتكوين أزمنة مختلفة، مثل المضارع التام.

● **الكلمات المفتاحية:** الأفعال ، الأفعال المساعدة ، افعال الكينونة ، الصفة.

## ■ Utangulizi

Kitenzi ni neno linaloeleza jambo lililotendwa au lililotendeka. Kitenzi huarifu lililofanyika au lililofanywa na kiumbe hai chochote kinachoweza kutenda jambo. Kitenzi cha Kiswahili huundwa na mzizi pamoja na viambishi vyenye uamilifu wa aina tofauti.

Kuna aina kuu tatu za vitenzi katika lugha ya Kiswahili: vitenzi vikuu, vitenzi visaidizi na vitenzi vishirikishi.

- vitenzi vikuu(T): vitenzi vikuu ni vile ambavyo hubeba ujumbe muhimu wa kiarifu cha sentensi.
- vitenzi visaidizi: hivi hutoa taarifa ya kusaidia vitenzi vikuu. Hutoa taarifa kama vile uwezekano, wakati, hali n.k. vitenzi visaidizi daima hutumika na vitenzi vikuu, ndivyo vinavyobeba viambishi vya wakati.
- vitenzi vishirikishi: hivi ni vitenzi ambavyo hufanya kazi ya kuunga sehemu mbili za sentensi. Havichukui viambishi vya nafsi, njeo, ama hali.

## ■ Vitenzi (T):

Kabla ya kufafanua kitenzi kishirikishi na kitenzi kisaidizi na dhima zake, lazima tufafanue kitenzi katika lugha ya Kiswahili na aina zake.

Vitenzi ni maneno yanayosimamia kitendo. Kila kitenzi huwa na shina la kitenzi (shina la kitenzi ni sehemu ndogo zaidi ya kitenzi ambayo ndiyo huwakilisha tendo hilo). Shina la kitenzi huambatanishwa na viambishi ili kutoa maana iliyokusudiwa kama vile mtendaji, mtendewa, wakati kitendo kinafanyika na pia kauli ya kitenzi hicho(Mgullu, R.S.1999).

Kuna ufafanuzi mwingine wa vitenzi unasema: Vitenzi ni maneno yanayoarifu kuhusu jambo linalotendwa au kutendewa nomino. Vitenzi huwa na mzizi ambao kwamba ndio unaosimamia tendo lenyewe na mzizi huo huambatanishwa na viambishi ili kuleta maana inayokusudiwa (Kimani Njogu na Dorothy K. Nganje2006). Kwa mfano:

Aliruka:

A-li- viambishi awali Ruk- mzizi a-kiambishi tamati

Vitenzi ni aina mojawapo ya aina ya maneno katika lugha. Umoja wa neno vitenzi ni kitenzi. Kitenzi kimefasiliwa na wataalamu mbalimbali. Kwa mujibu wa TUKI (1990) kitenzi ni neno ambalo huarifu tendo linalofanyika. Masamba na wenzake (2001) wanafasili kitenzi kama aina ya neno linalotoa taarifa juu ya tendo linalofanyika au linalotendwa na kiumbe au kitu. Habwe na Karanja (2004) wanafasili kitenzi kama aina ya neno linaloarifu jambo linalofanywa na mtu, mnyama au kitu kingine chochote. Aidha, Richards na wengine (1985) wanadai kuwa kitenzi ni neno ambalo hutokea kama njeo, hali, nafsi, idadi na dhamira katika kueleza tendo au hali. Kutokana na fasili za wataalamu hao, utafiti huu umefasili kitenzi kama neno linaloonyesha tendo au hali ya kutenda katika nomino. Kitenzi hubeba mambo muhimu ambayo ni tendo lenyewe linalotendeka, wakati tendo linapotendeka, hali ya kitenzi chenyewe, kauli ya kitenzi chenyewe na uyakinishi au ukanushi wa kitenzi chenyewe.

kuna aina kuu tatu za vitenzi katika lugha ya Kiswahili : vitenzi vikuu, vitenzi visaidizi na vitenzi vishirikishi (Masamba na wenzake,2001) Vitenzi vikuu hubeba taarifa ya tendo, hali ya tendo na kauli ya tendo.

Vyote hivi huundwa na mofimu zilizounda kitenzi. Vitenzi vikuu huwa na maana hata kama vikisimama peke yake, huweza kuonesha ukanushi na huundwa kwa mofimu mbalimbali. Kwa mfano neno anafundisha; taarifa ya tendo ni kuelimisha ambayo imeundwa na mofimu “fundisha”; hali ya tendo ni ya kuendelea ambayo imewasilishwa na mofimu “na” na kauli ya tendo ni ya kutenda ambayo imewasilishwa na mofimu “fundisha”.

Kitenzi kisaidizi ni kitenzi ambacho husaidia kitenzi kikuu kukamilisha sentensi. Kitenzi kisaidizi hakiwezi kuwa na maana iwapo kitasimama peke

yake. Hii ndio maana kinaitwa kitenzi kisaidizi kwani maana yake utaipata iwapo kitatumika na kitenzi kikuu. Mfano wa kitenzi kisaidizi ni alikuwa, alikwisha, angali, ingawa, kuja, kwisha na kadhalika (Rubanza, Y.I. 1996). Kitenzi kisaidizi hujulisha njeo, hujulisha uyakinishi au ukanushi na huundwa na mofimu mbalimbali. Sifa za Kitenzi kisaidizi ni kwamba hakikamilishi taarifa, mara zote huambatana na kitenzi kikuu katika kutoa taarifa na hudokeza nyakati mbalimbali za kutendeka kwa tendo( Rubanza, Y. I. 2006).

Kitenzi kishirikishi ni kitenzi ambacho huonyesha umoja wa vitu katika hali au tabia au katika mazingira ya aina moja. Mfano wa vitenzi vishirikishi ni kama vile alikuwa, si, ni, ndiyo siyo na kadhalika.

■ **Aina za vitenzi :**

● **Kitenzi kikuu:**

Ni kitenzi ambacho hutoa wazo kwa tendo ambalo linatendwa na nomino au kiwakilishi cha nomino. Mara nyingi kitenzi kikuu hukaa peke yake katika sentensi na hutoa taarifa kamili bila ya kuhitaji msaada wa kitenzi kingine na alama yake ya kiisimu ni (T).kwa mifano:

Ali anacheza mpira

wew unakula chakula

watoto hawa wamesoma kitabu

vyakula vimepikwa vizuri sana

Nyinyi mlisafiri Tanzania

Sifa za kitenzi kikuu katika lugha ya Kiswahili:

1-Huweza kusimama peke yake katika tungo au sentensi na kukamilisha taarifa bila ya kuwepo kitenzi kingine.

Mfano: Dada anasafisha

2- Huweza kuonesha ukanushi au uyakinishi

Mfano: Yeye anacheza (uyakinishi) Mimi sitakula chakula leo (ukanushi)

3-Huundwa kwa viambishi mbalimbali.

Mfano: Tu- ta- an- dik-a

● **Kitenzi kikuu kisaidizi :**

ni kitenzi ambacho hukaa sambamba na kitenzi kikuu ili kukisaidia kukamilisha taarifa. Kitenzi kikuu kisaidizi kikiwa peke yake hakiwezi kutoa taarifa kamili. Hivyo basi ni lazima kiambatane na kitenzi kingine (kikuu) ndipo taarifa yake ikamilike na alama yake ya kiisimu ni (TS).kwa mfano:

Kaka yangu alikuwa anafurahi sana.

(alikuwa ni kitenzi kisaidizi TS - na anafurahi ni kitenzi kikuu T).

Ali alikuwa anataka kwenda shambani kulima ardhi (alikuwa, anataka, na kwenda vyote ni vitenzi visaidizi isipokuwa kulima inabaki kuwa kitenzi kikuu

Watoto walikuwa wanataka kula chakula (walikuwa na wanataka vyote ni vitenzi visaidizi - isipokuwa kula ambapo hapa kimeainishika kama kitenzi kikuu). Kwa kawaida kitenzi kikuu hukaa mwisho hata kama nyuma yake kutakuwa na wasaidizi kumi.

Dhima za kitenzi kikuu kisaidizi:

Dhima za kitenzi kikuu kisaidizi zimegawanyika katika makundi makuu mawili - nayo ni:

1) Kujulisha njeo (njeo = wakati, nyakati)

2) Kujulisha uyakinishi na ukanushi wa tendo/matendo

Sifa za Kitenzi kisaidizi

- Hakikamilishi taarifa. Mfano, Kaka alikuwa

- Mara zote huambatana na kitenzi kikuu katika kutoa taarifa. Mfano, Upepo ulikuwa unavuma.

- Hudokeza nyakati mbalimbali za kutendeka kwa tendo. Yaani, wakati uliopo, uliopita na ujao. Mfano, Alikuwa, Atakuwa, n.k

● **Kitenzi kishirikishi :**

ni kitenzi ambacho hujulisha hali ya kuwepo au kutokuwepo kwa uhusiano/ ushirikiano baina ya vipashio vya lugha. Uhusiano huo unaweza kuwa katika tabia, hali, au mazingira fulani na alama yake ya kiisimu ni (t).kwa mfano:

Ali ni mvulana mwema

Mwalimu wetu si mkali

Yule ndiye mwanafunzi aliyeibuka wa kwanza

Aina za vitenzi vishirikishi:

Aina za vitenzi vishirikishi vimegawanyika katika makundi makuu mawili - navyo ni:

■ **Vitenzi vishirikishi vikamilifu:**

Ni maneno ambayo yamekamilika, yaani hayaambatanishwi na mofimu/ kiambishi / silabi / neno au kitenzi kingine. Vitenzi hivi pia hugawanyika katika makundi madogomadogo na alama yake ya kiisimu ni (t) ndogo.

Kuna mizizi sita ya vitenzi vishirikishi vikamilifu:

(i) -KUWA

Endapo utakuwa na kitenzi cha mzizi wa -kuwa kimesimama/kimekaa peke yake katika sentensi na kimetoa taarifa kamili - basi hicho ni kitenzi kishirikishi. Mifano:

Mohamed alikuwa mwanafunzi mtundu

Ali atakuwa mtu mzuri

Mohamad Hasan alikuwa mwimbaji hodari sana

Wewe hukuwa mlevi

Nyinyi Mtakuwa wanafunzi bora

(ii) NI

Hiki ni kitenzi kishirikishi kinachojulisha uyakinishi wa tendo. Kitenzi

hiki hujulisha kuwepo kwa uhusiano baina ya vipashio vya lugha. Mifano:

Ahmed ni mwanafunzi

Simba ni mnyama mkali

Mimi ni mwalimu

Sisi ni walibya

(iii) SI

Hiki ni kitenzi kishirikishi kinachojulisha ukanushi wa tendo. Kitenzi hiki hujulisha kuwepo kwa uhusiano baina ya vipashio vya lugha. Mifano:

Ahmed si mwanafunzi

Simba si mnyama mkali

Mimi si mwalimu

Sisi si walibya

(iv) Vitenzi vishirikishi vinavyojulisha umiliki

Hivi ni vitenzi vinavyotoa taarifa ya umiliki kwa nomino au kiwakilishi. Mifano:

Fatima ana gari zuri

Chakula kina chumvi nyingi

Ulimi hauna mfupa

Darasa letu lina vumbi

Chatu hana meno

(v) Vitenzi vishirikishi vya viambishi vya mahali (po, mo, ko)

Hivi ni vitenzi vinavyotoa taarifa ya mazingira ya tendo husika. Mazingira hayo ni pamoja na kuwa nje, ndani, juu ya, au katika eneo fulani. Mifano:

Ndoo imo kisimani

Kikombe kiko mezani

Wanafunzi wamo darasani

Yeye yumo chumbani

Fedha zimo kabatani

Jembe lipo shambani

(vi) Kitenzi kishirikishi chaa viambishi vya ngeli vikisimama peke yake

Hivi ni vitenzi vinavyobainisha maana ya ngeli ikisimama peke yake. Mifano:

Ndoo ikisimani

Kikombe ki mezani

Wanafunzi wa darasani

hapa ni lazima sauti ibadilike ili kutoa maana tofauti na ile maana ya kiwakilishi/kivumishi cha -a unganifu). Bimaana ya kwamba wakati unataja wanafunzi wa - kwenye wa lazima ufanye kama unasimama vile:

Fedha zi kabatani

Jembe li shambani

■ **Vitenzi vishiriki vipungufu:**

Ni vitenzi chenye mzizi wa NDI-. Vitenzi hivi hujulisha msisitizo wa jambo. Vitenzi vishirikishi vipungufu huchukua viambishi vya nafsi na viambishi vya ngeli vya urejeshi na alama yake ya kiisimu ni (t) pia.

Kuna mizizi miwili ya vitenzi vishirikishi vipungufu. Navyo ni mzizi wa nafsi na ngeli za urejeshi.

(i) Nafsi

| Nafsi | Umoja | Wingi |
|---|---|---|
| I | Mimi | Sisi |
| II | Wewe | Ninyi/nyinyi |
| III | Yeye | Wao |

Mifano:

Mimi ndimi mwalimu wao

Sisi ndisi walimu wao

Wewe ndiwe nwalimu wao

Ninyi ndinyi walimu wao

Yeye ndiye mwalimu wao

Wao ndio mwalimu wao

(ii)Vya ngeli vya urejeshi

Mifano:

Hizi ndizo ndizi zake

Hiki ndicho kitabu chake

Hili ndilo shamba lao

Humu ndimo alimoingia

Hapa ndipo anapoishi

Huku ndiko alikoenda

■ **Hitimisho**

Kutokana na makala hii, ni dhahiri kuwa vitenzi katika lugha ya Kiswahili hutofautiana na baadhi ya lugha nyingine kulingana na muundo na kazi yake, ingawa vinafanana navyo katika neno.

vitenzi ni maneno yanayoelezea kitendo au mazungumzo juu ya jambo linalotokea

Kitenzi kisaidizi kinachukuliwa kuwa mojawapo ya aina muhimu zaidi za vitenzi. Inachukuliwa kuwa sehemu ya pili ya aina za vitenzi. Ya kwanza, kama tulivyojifunza, inaitwa kitenzi cha msingi, ikimaanisha kuwa ni kitenzi cha msingi cha sentensi na ni muhimu, bila ambayo sentensi haina maana. Kuhusu kitenzi kisaidizi, ni kitenzi kinachokuja kusaidia kitenzi kikuu.

Kumaanisha kuwa ni kitenzi cha pili katika sentensi.

Kinachojulikana kama kitendo shirikishi ni kitendo kinachoonyesha umoja wa mambo katika hali, tabia, au katika mazingira sawa kwa maana nyingine Vitenzi vinavyoshirikisha vitu kihali, kitabia au kimazingira .

### ■ Marejeleo


1- Mgullu, R. S. (1999). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahii.Nairobi:* Longhon Publishers.

2- Kimani Njogu na Dorothy K. Nganje2006, Kiswahili kwa vyuo vya ualimu, Jomo Kenyatta Foundation, Nairobi, Kenya.

3- TUKI, (1990), Kamusi ya Isimu ya Lugha , Dar es Salam, Tanzania, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

4- Massamba, D. P. B., Y. M. Kihore na J. I. Hokororo (2001), *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA); Secondari na Vyuo. Dar es Salaam:* TUKI. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

5- Habwe, J. Na Karanja, P. (2004). Misingi ya Sarufi ya Kiswahili. Nairobi. Phoenix Publishers Limited.

6- Richards, J., Platt, J. na Weiber, H. (1985). Longman Dictionary of Language and Teaching Applied Linguistics. Edinburgh Gate: Pearson Education Ltd.

7- Rubanza, Y. I. (2006). *Vidokezo vya Mofolojia ya Kitenzi katika Luzinza.Kioo cha Lugha*, *4*(1).

8- Rubanza, Y.I. (1996). *Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam. Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

9- https://sw.wikipedia.org/wiki/Vitenzi_vishiriki_vipungufu

10- https://swa.gafkosoft.com/vitenzi

11- https://www.jamiiforums.com/threads/aina-za-vitenzi-t-katika-lugha-ya-kiswahili.1886827/